# PRECIOUS STAR EXAM SERIES

# DARASA LA NANE MWAKA WA - 2022

{003}

# KISWAHILI : LUGHA

{8}

*Muda: Saa 1 Dak. 40*

**SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO**

1. Umepewa karatasi hii ya maswali na karatasi ya kujibia. Karatasi hii ina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika karatasi hii.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika hii ya maswali

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

4. Tumia penseli ya kawaida
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo umeandika katika karatasi ya majibu

   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**

   **JINA LAKO**

   **JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotegea mwanzo wa karatatsi ya majibu
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.
9. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D, Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari kwenye kisanduku chenye herufi uliochagua kuwa ndilo jibu.

    **28.** Jibu mwafaka la "Lala salama" ni ________

    A. salmini B. nawe pia C. aheri D. asante

    Jibu sahihi ni **B**

    **11.** [A] [B] [C] [D] **15.** [A] [B] [C] [D] **17.** [A] [B] [C] [D] **28.** [A] ~~[B]~~ [C] [D]

    Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 25, kisanduku chenye herufi **B** ndicho kilichochorwa kistari

11. Chora kistari chako vizuri, kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne uliovyopewa.

**Kitabu hiki cha maswali kina kurasa 6 zilizopigwa chapa**

**Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi, umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi .**

Katika ___1___ wa habari ni ___2___ msamiati unaotumika ufahamike ___3___ na pande ___4___ mbili. Pia katika ___5___ ni lazima ___6___ mtafsiri ___7___ mwandishi pamoja na dhamira aliyokuwa nayo. ___8___ ya hayo afahamu mapenzi ya ___9___ iliyolengwa.

1. A. upeanaji B. upashanaji C. utoaji D. upitiaji
2. A. shati B. kweli C. sharti D. kuwa
3. A. pima B. pema C. shwari D. barabara
4. A. zote B. sote C. nyote D. zozote
5. A. kutafsiri B. kutafusiri C. kunena D. maongezi
6. A. pawe B. kama ibada C. kuwa D. kama mchana
7. A. amuelewe B. awaelewe C. amwelewe D. asielewe
8. A. Minghairi ya B. Aghalabu C. Maadamu D. Fauka ya
9. A. adhira B. mwandishi C. hadhira D. watu

Alivimba ___10___ na kujiona bora zaidi ___11___ ___12___ wenzake. Hayo yalitokana na sifa ___13___ alizomiminiwa na walimu na wavyele. Kudurusu akaacha. Mwishowe alianguka ___14___ sana. Ama kweli ___15___.

10. A. mguu B. kichwa C. mkono D. mwili
11. A. kuliko B. kuwaliko C. mbele D. zaidi
12. A. watoto B. washindi C. watahini D. watahiniwa
13. A. mpwitompwito B. kadhaa C. mbelele D. belele
14. A. chali B. pu C. vibaya D. kifudifudi
15. A. aisifuye mvua imemnyea C. mwenda omo na tezi, marejeo ngamani C. mjinga mvishe kilemba uone mwendowe D. asiyekuwapo na lake halipo

**Kutoka swali la 16 mpaka 30, jibu kila swali ukifuata maagizo uliyopewa.**

16. **Andika wingi wa:-**
Dawa yake ya kulevya ninaitumia.
A. Madawa yao ya kulevya twayatumia
B. Dawa zake za kulevya tunazitumia
C. Dawa zao za kulevya tunazitumia
D. Dawa zao za kulevya twazitumia

17. Pambo la kidani huvaliwa wapi?
A. Mkononi
B. Mguuni
C. Shingoni
D. Kwenye sikio

18. Chagua sentensi ambayo ina kivumishi kimilikishi
A. Mtoto wangu amepita mtihani
B. Mpishi amepika chakula kitamu
C. Choo kinanuka fee!
D. Daktari ametibu wagonjwa watatu

19. **Sanifisha kauli hii kwa kutumia kiashiria radidi:-**
Uyoga _________ haukatiki kamwe.
A. uo huo
B. huo uo
C. huo huo
D. uo uo

20. Chagua jibu la adabu lisilo sahihi
A. hodi - Kongoni
B. Kwaheri - Ya kuonana
C. Pole - Asante
D. Karibu twala - Starehe

21. Chagua jibu ambalo kiumbe hakijaambatanishwa na makazi yake;
A. kuku - zeriba
B. nyuki - mzinga
C. konokono - kombe
D. nyuni - kiota

22. Tambua sentensi yenye kiambishi ngeli **'ki'** iliyo sahihi;
A. Watakimbizana leo
B. Akija tumfuate
C. Atacheza kitoto
D. Alikitupa chote

23. Ni orodha gani yenye ndege wa kufugwa?
A. Bundi, kasuku, batamzinga, njiwa
B. Heroe, bukini, njiwa, bundi
C. Kigogota, shore, kasuku, kanga
D. Bukini, njiwa, bata, kuku

24. **Kamilisha:-**
Mpira wa wavu pia huitwa
A. mpira wa pete
B. mpira wa voliboli
C. mpira wa kikapu
D. mpira wa magongo

25. Chagua orodha iliyo na nomino zinazolingana
A. mwanahewa , kivuko, pilipili
B. kitenge. kitegauchumi, uchumi
C. mwanasesere, batamzinga, kinasasauti
D. kitindamimba, kilembwe, kining'ina

26. Ambatanisha maumbo na majina mtawalia



A. Mistari sulubu, tao, wimbi
B. Kiegema, hilali, zigizagi
C. Mistari sambamba, hilali, zigizagi
D. Mistari sambamba, kopa, mstari wimbi

27. **Bainisha matumizi ya methali:-**
Mti hubomolewa na tundaze
A. Mtu mkubwa akija kukosa hali wanaomtegemea hawana heri
B. Yeyote akiteleza maishani kwenda jongomeo ni rahisi
C. Mti ukianguka ni lazima uyaathiri matunda machache
D. Mtu akifa huacha wanawe kuendeleza mambo

28. Ambatanisha maelezo haya
A. Mloto - mshororo wa tatu katika ubeti
B. Mleo - mshororo wa pili katika ubeti
C. Tasdisa - shairi la mishororo mitatu
D. Ukwapi - kipande cha kwanza cha mshororo

29. Chagua neno lisiloonyesha hali ya udogo
A. kibanda
B. kijumba
C. kijiji
D. kiguu

30. Ni sentensi gani yenye kitenzi katika kauli ya kutendesha?
A. Kuimbizana kwao ni kuzuri.
B. Kwa nini walipigiana wanao.
C. Sijui kwa nini wamlize mtoto?
D. Waliogeshana baharini kwa maji ya chumvi.

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali 31 - 40.**

Bwana Mapuya alikuwa mlevi wa kutajika kitongojini mwake. Hakuna aliyekosa kusimulia kisa cha mzee huyu. Mapuya hakusifiwa tu na wapiga maji wenzake kwa umahiri wake katika kuubugia uji mchachu bali pia alisifika na watoto na vijana wa kijijini kwa sauti yake ya ninga hasa alipokuwa ameonja zake mbili tatu.

Mapuya alikuwa manamba katika shamba moja la mkwasi aliyepanda maua kwa madhumuni ya kuyauza ughaibuni. Mshahara wa Mapuya haukuwa wa kumezewa mate wala haukuwa wa kutemewa mate, maadamu yeye ndiye aliyekuwa msimamizi wa shamba hili. Kipato chake kingeweza kuikidhi aila yake ya watoto watatu na mke mmoja ambaye pia alichapa kazi katika konde la mkwasi yuyu huyu. Hata hivyo, **Mapuya alikuwa daima yu waya**. Kila mwisho wa mwezi ulimwengu mzima ulimtambua. Alikuwa na hulka ya kujilawa alfajiri na mapema Ijumaa ya mwisho wa mwezi kuenda kuutwaa mshahara wake. Papo hapo, Mapuya angeshika njia hadi kwa mgema maarufu katika mtaa wao na kupiga kachombe kwenye vidimbwi vya pombe hadi misuli ya tumbo lake ilipochoka na kulalamika. Mwishowe, Mapuya angekuwa hana hanani, na kumrudia maskini mkewe, uso kauinamisha kwa tahayuri.

Nyumbani mkewe, mama Subira angepata kibarua kiingine cha kumwuguza simba wake kwa siku kadhaa kabla yeye Mapuya hajarudi kazini. Ilimbidi Subira kuyatibu maradhi ya Mapuya ambayo hayakusikia dawa nyingine ila mchuzi wa nyama. Subira alijibidiisha kwa vyovyote vile kumtibu mumewe huyu, hasa siku za mwanzo mwanzo. Baadaye stahamala ilianza kumwishia hasa alipogundua kuwa mzigo wa malezi ya wanawe alimlemea yeye. Alianza kumrai mumewe auache mchezo huo ambao ulitishia kumfanya aumwage unga wake na kudhoofisha afya yake ambayo tayari ilikuwa ikididimia. Hata hivyo maneno ya Subira yaliangukia moyo wa jabali lisilosikia la mwadhini wala la mteka maji msikitini.

Mapuya **alikataa katakata** kuuacha uraibu wake huku akidai kwamba mume asiyeonja vileo hayamudu maendeleo na kwamba asingekubali kudhibitiwa na mkewe asilani.

Baada ya kukata tamaa Subira alikata shauri kumwendea mshauri mmoja aliyekuwa na kliniki hapa mtaani ili kuililia hali yake. Mshauri huyu alipozungumza na Mapuya, Mapuya alijawa na hamaki. Akalalamika kuwa mkewe alikuwa amemvua nguo hadharani na kuapa kumpatiliza. Jioni hiyo chengoni mwa Mapuya mlisikika kilio kikubwa zaidi ya kile cha kawaida. Ingawa majirani walikuwa kila siku wakiamua kujitia za mtonga, vilio vya watoto viliwatia imani, wakaamua kumkabili hasidi huyu. Mapuya akaombwa kuufungua mlango lakini akachagiza kuwa haikufaa majirani kuyaingilia mambo yake ya unyumba. Hata hivyo, shinikizo lilipozidi, alifungua, akatoka na kujiendea zake kumwacha Subira kumwaga kuku mtama.

Subira aliwaelezea majirani masaibu aliyokuwa ameyapata. Akawasimulia jinsi Mapuya alivyoitelekeza familia yake asijue njaa wala shibe yao. Watoto tayari walikuwa wamefukuzwa shule kwani Subira hakuweza kulipa karo tena. Aidha, madeni ya mumewe alilipa yeye sasa ndipo akapata kipigo kwa kumwendea mshauri alipohisi amefika ukingoni.

Baadaye, mmoja wa majirani alimshauri Subira kumwendea mwajiri wake ambaye alisikitika sana na kukashifu kutowajibika kwa Mapuya. Alimwita Mapuya mbele ya mkewe na jirani yake. Alimfahamisha kwamba ingebidi, ama akubali robo tatu ya mshahara wake uwaendee wanawe hadi pale atakapobadilika au ajiuzulu kazi. Mapuya alikubali shingo upande na kutokana na fedheha, aliutupa ulevi jongoo na mti wake.

**31.** Kulingana na aya ya kwanza
- A. Mapuya alisifiwa zaidi na walevi wenzake
- B. ulevi wa Mapuya na kuiga mambo kulimfanya kujulikana
- C. Mapuya alisifiwa na walevi, watoto na hata vijana
- D. ulevi wa Mapuya haukumtatiza yeyote pale kijijini

**32.** Bwana Mapuya alikuwa na wadhifa gani pale shambani?
- A. Alikuwa mkurugenzi
- B. Alikuwa meneja
- C. Alikuwa kondakta
- D. Alikuwa mkadamu

**33.** **Mapuya alikuwa daima yu waya** ina maana kuwa
- A. mara nyingi alikuwa hana pesa zozote
- B. sanasana aliendа kazini akiwa mlevi
- C. mara nyingi Mapuya hakuonekana kazini
- D. aghalabu hakuenda nyumbani baada ya malipo

**34.** Ni kweli kusema kwamba
- A. Mapuya alikuwa akiugua kila mwisho wa mwezi baada ya kulewa
- B. Mapuya alimshurutisha mkewe kumnunulia nyama akisingizia ugonjwa
- C. Mapuya alitumia pesa zilizobaki kulewa baada ya kukidhi mahitaji ya familia
- D. Mapuya alimpokonya mkwewe mshahara wake na kuutumia ulevini mwake

Teacher.co.ke

35. Yapi hayakuwa madhara ya ulevi wa Mapuya?
A. Kumletea matatizo ya kiafya
B. Kumtishia kuipoteza amali yake
C. Kumsababisha kuitelekeza aila yake
D. Kuwa maarufu kote kijijini kwao

36. Mapuya **<u>alikataa katakata</u>** kuuacha uraibu wake. Maneno yaliyopigwa mstari yanaonyesha fani gani ya lugha?
A. Istiara
B. Nahau
C. Tanakali za sauti
D. Vielezi vya mkazo

37. Kwa nini Bwana Mapuya alimwadhibu sana mkewe jioni hiyo?
A. Mkewe alikuwa amemsihi kuuacha ulevi
B. Alihisi kwamba mkewe alikuwa amemwaibisha
C. Ilikuwa ada yake kumpiga mke na watoto alipolewa
D. Mkewe alikuwa ameanza kuyaingilia maisha yake

38. Mlango ulipofunguliwa
A. Mapuya alimwacha mkewe akiwaelezea majirani yaliyojiri
B. mke alitoka nje na kuumwaga mtama wao
C. Mapuya alijibizana na majirani kwa kijidukiza katika mambo yake
D. Mke aliwasimulia majirani nao wakamvamia Mapuya kwa maneno

39. Ni makosa kusema kuwa
A. Subira ndiye aliyelipa karo ya wanawe
B. huenda majirani hawakujua chanzo cha mgogoro
C. Subira alizoea kuwaendea washauri alipotaabika
D. Mapuya hakuyajali mahitaji ya familia yake

40. Kwa nini Mapuya akaamua kuuacha uraibu wake hatimaye?
A. Aligundua kuwa angeipoteza kazi yake
B. Mshahara wake ulikatwa akaachiwa robo tu
C. Alishurutishwa kuiacha kazi ama apigwe kalamu
D. Alitambua kuwa ulevi wake ulimletea aibu

**<u>Soma ufahamu ufuatao kwa makini kisha ujibu maswali 41 - 50.</u>**

Mavazi humtukuza mtu hata humtweza. Hii hufungamana na vazi alilovaa, hadhara iliyopo, wakati na hata cheo cha mvaliaji. Ni fahari kubwa wala si aibu kwetu kuvalia nguo zetu za kienyeji wakati wa sherehe, mazishi ama mnasaba unaofaa. Wabunge wetu hulazimishwa kuvaa suti na tai na kaunda suti wanapokuwa bungeni. Hii haimanishi kuwa shati maridadi au suruali iliyopigwa pasi vizuri hudunisha hadhi ya mvaliaji. Bali vazi rasmi bungeni ni suti ya Ulaya kama vile wanafunzi wa kila shule wanayo sare yao maalum.

Kutothamini mavazi yetu ya kienyeji ni kukosea kwani yalikuwa na yangali na haiba yake ya mvuto wake maaluum na pia hisia za kizalendo. Vilemba, shanga na mgwisho ni mavazi ambayo yalikuwa na maana kubwa katika vyeo vya wazee wetu kwani yalikuwa yakionyesha heshima na umri wa mtu. Lakini leo mambo yako shaghalabaghla! Hata yale mavazi ya kawaida hayajulikani ya mume wala mke. Vijana hudai kuwa kiingiacho mjini si haramu hasa kikiwa kimetoka nchi za ng'ambo. Ndiposa wasichana huvaa kaptula, suruali ndefu, na kunyoa nywele kama vijana wa kiume. Si ajabu hivi karibuni kuwaona wavulana wakivaa rinda ama sketi kwani tayari wameanza kutobolewa maskio na kusuka nywele zao.

Jambo la kupendeza na kuvutia mno ni kule kuwaona Waafrika wa Afrika magharibi wakivalia nguo zao za kienyeji zenye mvuto wa ajabu wanapohudhuria mikutano ya kimataifa. Hali kadhalika, haya pia tunayaona kwa Wahindi, Waarabu, Wajapani na Waganda. Hawa hufanya hivyo kwa sababu wanaelewa kuwa mwacha asili ni mtumwa. Ingawaje tumeambiwa mcha Mungu si kilemba cheupe inatupasa tuvae nguo zinazotupa heshima na taadhima.

41. Shuleni wanafunzi lazima wavae

A. sare iliyopangwa

B. suruali, shati na viatu

C. nguo za heshima

D. nguo za kupendeza

42. Ni makosa kuyadharau mavazi yetu ya kienyeji kwa sababu

A. yalikuwa ya bei rahisi

B. wazee huyavaa

C. yanatupendeza mno

D. mwacha asili ni mtumwa

43. Kulingana na taarifa mwandishi

A. anataka watu wawe na uhuru wa kuvaa wapendavyo

B. anapendelea mavazi ya kimagharibi

C. anahimiza tuwe na vazi letu rasmi

D. anahimiza wabunge wavae suti ghali za heshima

44. ***"Kiingiacho mjini si haramu"*** ni msemo unaomaanisha

A. hakuna kilicho haramu

B. kufuata mabadiliko ya wengi ya kisasa

C. watu wa mjini hawana dhambi

D. cha kuokota mjini si haramu

45. Waafrika wa Afrika magharibi huvaa nguo za kienyeji ili

A. wadumishe utamaduni wao

B. wavutie wale wanaokutana nao

C. watambulikane kwani ni za bei ghali

D. wasionekane kwamba ni Waafrika

46. Chagua jibu ambalo si sahihi kwa mujibu wa taarifa

A. Ni wasichana tu ambao wamepotoka kimavazi

B. Nguo za kienyeji huashiria uzalendo

C. Waafrika bado wanatawaliwa kiakili

D. Mavazi ya kienyeji yanapendeza na kuvutia

47. ***"Kumcha Mungu si kilemba cheupe"*** ni msemo unaomaanisha

A. mcha Mungu avae kilemba cha rangi nyingine

B. anayevaa kilemba cheupe hamchi Mungu

C. mtu asiye na kilemba si mcha munga

D. kumcha Mungu ni moyoni si mavazi

48. ***"Shaghalabaghla"*** inamaanisha

A. shughuli nyingi

B. mavazi tofauti tofauti

C. kukosa utaratibu maalum

D. kuvaa nguo za kimagharibi

49. Mavazi ya kienyeji yanapaswa

A. kuvaliwa na wazee tu

B. kuuzwa kwa bei ya chini

C. kutodunishwa na kutodharauliwa

D. kuagizwa kutoka nchi za ng'ambo

50. Kichwa kifaacho zaidi kwa taarifa hii ni

A. Mavazi ya vijana

B. Mavazi ya kidini

C. Mavazi ya kimagharibi

D. Mavazi ya utamaduni